**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA YA 290)**

**<u>SHERIA NDOGO</u>**

**(Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1))**

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA ZA MWAKA, 2023**

*Jina* 1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Ushuru wa Mazao za Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, 2023.

*Matumizi* 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Tandahimba, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la serikali.

*Tafsiri* 3. Katika Sheria Ndogo hizi, bila ya kuathiri fasili katika Sheria nyingine maneno yafuatayo yatakuwa na maana iliyotajwa hapa:-

"**Afisa Muidhiniwa**" maana yake ni Afisa yeyote wa halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi;

"**Gulio**" maana yake ni eneo au sehemu yoyote ya wazi au iliyojengwa ambayo imetengwa na halmashauri kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua mazao na bidhaa zingine za viwandani, na itamaanisha pia Chama cha Ushirika cha Msingi kilichoteuliwa kuuza mazao mchanganyiko;

"**Halmashauri**" maana yake halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba;

"**Mazao mchanganyiko**" maana yake ni pamoja na mazao ya chakula, biashara na mazao ya misitu na Maliasili ambayo huzalishwa na kupatikana katika eneo la halmashauri, isipokuwa zao la korosho;

"**Mkurugenzi**" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, au mtumishi mwingine wa Halmashauri ambaye atateuliwa kukaimu nafasi hiyo;

“**Mnunuzi**” maana yake ni mtu, kikundi cha watu au taasisi yoyote inayojishughulisha na ununuzi wa mazao mchanganyiko katika eneo la halmashauri kwa nia ya kufanya biashara;

“**Msafirishaji**” maana yake ni mtu binafsi, kampuni, taasisi, au shirika ambaye anasafirisha mazao mchanganyiko;

“**Muuzaji**” maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi inayojishughulisha na uuzaji wa mazao mchanganyiko katika eneo la halmashauri;

“**Ushuru**” maana yake ni malipo yanayotozwa na kulipwa kwa Halmashauri kama kodi ya bidhaa au huduma inayotolewa;

“**Wakala**” maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, Kampuni au Shirika ambalo litakuwa limepewa mamlaka na Halmashauri ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri

“**Waziri**” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

*Ushuru wa mazao mchanganyiko*

4. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza au kununua mazao mchanganyiko katika eneo ambalo si gulio

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao mchanganyiko kwa kiwango cha **asilimia tatu (3%)** ya bei ya kununulia mazao kwa ajili ya mazao yote yanayosafirishwa katika eneo lake  kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(3) Ushuru huo utalipwa na mnunuzi kabla ya kusafirisha mazao.

(4)Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kununua au kusafirisha mazao bila kulipia ushuru.

*Wajibu wa kulipa ushuru*

5. (1) Ni marufuku kwa mnunuzi kununua mazao katika eneo la Halmalshauri bila kuwa na leseni halali ya biashara iliyoidhinishwa na halmashauri.

(2) Kutakuwa na kibali maalum cha kusafirishia mazao kwa mujibu wa Nyongeza ya Sheria Ndogo hizi, na ni marufuku kwa msafirishaji kupokea na kusafirisha mazao ambayo hayakulipiwa ushuru kwa kiwango kilichotajwa chini ya Sheria Ndogo hii.

(3) Ushuru unaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au wakala wake ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo cha malipo hayo.

(4) Ni wajibu wa mtu yeyote anayelipa ada au ushuru kudai na kuhakikisha anapewa stakabadhi halali ya halmashauri kwa malipo anayotoa.

*Wajibu wa mnunuzi*

6. (1) Kila mnunuzi atasaini mkataba na Halmashauri utakaomruhusu kununua na atapewa kibali na halmashauri.

(2) Mnunuzi ambaye ana wasaidizi atawajibika kuwatambulisha rasmi wasaidizi wake hao kwa Halmashauri kabla ya kupewa kibali.

(3) Ununuzi utafanyika katika maghala ya halmashauri au gulioni kwa mzani au kipimo chochote kingine kilichothibitishwa na Halmashauri au mamlaka nyingine iliyowekwa kisheria.

*Stakabadhi za malipo*

7. (1) Kutakuwa na stakabadhi zilizohakikiwa na Halmashauri na kila mnunuzi atatumia stakabadhi hizo wakati wa ununuzi wa mazao.

(2) Itakuwa ni haki ya mlipaji kuonyeshwa kitambulisho na Afisa mwidhinishwa au wakala kabla ya kulipa ada au ushuru wowote.

(3) Utakuwa ni wajibu wa mlipaji kuhakikisha anapewa stakabadhi ya malipo yoyote anayofanya

*Muda wa ununuzi*

8. Isipokuwa kwa ruhusa maalum ya maandishi iliyotolewa na Mkurugenzi:

(a) Ni marufuku kuuza na kununua mazao kabla ya saa kumi na mbili (12:00) asubuhi na baada ya saa kumi na mbili (12:00) jioni.

*Makosa*

9. (1) Litakuwa ni kosa chini ya sheria ndogo hizi kwa mtu yeyote;

(i.) ambaye kwa namna yeyote ile atamsaidia mnunuzi kukwepa ushuru.

(ii.) kukwepa kwa makusudi kulipa kiwango cha ushuru anachostahili kulipa

(iii.) kushawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ushuru.

(iv.) kwa mtu yoyote kujifanya msaidizi wa mnunuzi kununua mazao bila maagizo au usimamizi wa mnunuzi.

(v.) kwa mtu yeyote kukataa au kushindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Mkurugenzi kuhusiana na ulipaji wa ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi

(vi.) kumzuia Afisa mwidhiniwa au wakala kukusanya ushuru au kufanya jambo lolote jingine katika kutekeleza majukumu yake chini ya sheria ndogo hizi.

*Adhabu*

10. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (**200,000.00**) na isiyozidi Shilingi Milioni Moja **(1,000,000.00)** au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini

na nne au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

| | | |
|---|---|---|
| *Kukusanya ushuru kwa kukamata mali* | 11. | (1) Bila ya kuathiri masharti yanayotajwa katika kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo ndogo hizi, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata na kushikilia mali za mdaiwa, zinazosafirishwa bila kulipiwa ushuru, zenye thamani sawa na ushuru anaodaiwa au zaidi, kiasi hicho kikihesabiwa pamoja na gharama za zoezi la ukamataji na usafirishaji wa mali hiyo.<br><br>(2) Halmashauri itatoza faini ya shilingi 5,000 kwa kila kilo moja ya mazao yaliyozidishwa bila kulipiwa ushuru au itauza kwa mnada mali yoyote iliyokamatwa chini ya Sheria Ndogo hii iwapo;<br><br>(a) baada ya siku saba (7) tangu mali kukamatwa mdaiwa hajalipa ada ama ushuru anaodaiwa, pamoja na gharama za ziada anazopaswa kulipa,<br>(b) mali iliyokamatwa inaweza kuharibika haraka, ndani ya kipindi kisichozidi siku mbili za kalenda,<br>(c) mmiliki wa mali iliyokamatwa hatakuwa amejitokeza ndani ya siku saba baada ya mali yake kukamatwa. |
| *Mipaka ya uwajibikaji wa Halmashauri* | 12. | Halmashauri haitawajibika kwa namna yoyote na kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni ya ushuru au kwa mali zitakazokamatwa na kushikiliwa chini ya Sheria ndogo hizi. |
| *Uwezo wa Mkurugenzi.* | 13. | (1) Mkurugenzi kwa maandishi anaweza kumuagiza mnunuzi au mzalishaji yeyote aandae na kukabidhi kwake taarifa ya kiasi cha mazao alichozalisha au kununua katika kipindi kinachotajwa katika agizo hilo. |

(2) Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kumteua Afisa yeyote wa Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

(3) Bila ya kuathiri kifungu cha 13(1) ya Sheria Ndogo hizi, Afisa yeyote wa Halmashauri atakuwa ni Msimamizi wa hizi Sheria Ndogo.

(4) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumteua Wakala kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

*Uwezo wa kufifilisha kosa*

14. Mkurugenzi au Afisa Muidhiniwa anaweza kumtoza faini isiyozidi Elfu Hamsini (50,000/=) mtu yeyote aliyetenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa mujibu wa nyongeza ya Sheria Ndogo hizi.

**NYONGEZA**

**KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO**

Namba ya kibali…………………….. Tarehe ……………………...

Msimu…………………………. Zao ………………………

Jina la mnunuzi………………………………………………………………..

Idadi ya Tani/Kg za awali…………………………………………………………

Kiasi kilichonunuliwa……………………………………………………………

Jumla ya Tani/Kg………………………………………………………………….

Kiasi kinachosafirishwa…………………………………………………………

Kiasi kilichobaki………………………………………………………………..

Namba ya stakabadhi ya ushuru……………………………………………………..

PDN ya chama cha msingi/Stakabadhi…………………………………………………

Tarehe ya kusafirisha…………………………………………………………..

Jina la Dereva…………………………………Na. ya Gari……………………………

Jina la Afisa aliyeidhinisha mzigo………………………….Saini………………………

……………………………………………………

Mhuri na saini ya Mkurugenzi/Mweka hazina

| | | |
|---|---|---|
| 15. | Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio lililopitishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba katika kikao kilichoketi na kufanyika tarehe……………………… na ilibandikwa mbele ya:<br><br>…………………………………<br>**MARIAM SAID MWANZALIMA**<br>*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*<br><br>…………………………………<br>**BAISA ABDALLAH BAISA**<br>*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*<br><br>**NAKUBALI**<br>**…………………………………………………**<br>**ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB)**<br>**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS**<br>**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA)**<br>**Dodoma,**<br>**Julai, 2023** | *Lakiri ya Halmashauri* |